**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2002**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (40 Alama)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Taja tofauti nne kati ya kitabu cha kiada na kitabu cha ziada.

2. Eleza mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wachezaji wanaposhiriki michezo.

3. Fafanua misingi minne ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.

4. Toa maana ya istilahi zifuatazo:

   (a) ujuzi

   (b) lengo kuu

   (c) mada ndogo

   (d) lengo mahsusi.

5. Eleza stadi nne muhimu anazotakiwa kuwa nazo mwalimu ili kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia papo kwa papo.

6. Taja njia nne zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenye tabia tofauti.

7. Eleza vipengele vinne vya muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

8. Taja mambo manne yanayozingatiwa na mwalimu kabla ya kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.

9. Eleza stadi nne za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo.

10. Taja aina nne za zana za upimaji zinazotumika kupima ujifunzaji.

## SEHEMU B (40 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii.

11. Changanua umuhimu wa maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia.

12. Jadili nafasi ya zana za kufundishia na kujifunzia katika mchakato wa ujifunzaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

13. Eleza faida na changamoto za upimaji na tathmini katika somo la Haiba na Michezo.

14. Tathmini hatua zinazopaswa kufuatwa na mwalimu katika maandalizi ya somo la Haiba na Michezo.

**SEHEMU C (20 Alama)**

Jibu maswali mawili katika sehemu hii.

15. Fafanua changamoto zinazokumba maandalizi na matumizi ya zana za kufundishia.

16. Eleza misingi ya ufundishaji na jinsi inavyosaidia mwalimu kufanikisha somo.

17. Jadili nafasi ya kiongozi cha mwalimu katika maandalizi ya somo.

18. Eleza mchango wa somo la Haiba na Michezo katika kumjengea mwanafunzi maadili na mshikamano wa kijamii.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org